# MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

***Karatasi ya maswali: namba 2***

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa ‘Kazi ya ziada’ unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

**MASOMO: 5 – 8**

5. A. Uhai ulianzaje duniani?
   B. Eleza jinsi mwanadamu wa kwanza, Adamu, alivyoumbwa.
   C. Kumbukumbu la Torati 4: 15 – 19 linatuambia nini?
   D. Ibada za sanamu kwa sasa zipo kwa namna gani?

6 A. Sema kama semi zifuatazo ni Kweli au ni Uongo

a) Sisi wote tunao wema fulani ndani yetu.
b) Imani maana yake ni kuamini.
c) Adamu alibidi afe kwa kuwa alitenda dhambi.
d) Yesu hakufanya dhambi kamwe.
e) Adamu alikwenda mbinguni alipokufa.

*Kazi ya ziada:*
6 B. Katika Isaya 20 kuna maelezo juu ya mateso na kifo cha Yesu. Andika mambo matatu yanayosemwa kumhusu Yesu na mawili yanayosemwa kutuhusu sisi.

7 A. Yesu Kristo yupo wapi sasa?

7 B. Yesu atakaporudi hapa duniani:

a) Nini kitawatokea waumini wa kweli waliokwisha kufa?
b) Nini kitawapata waovu?

8 A. a) Ni nini unafikiri ni ishara ya maana kuliko zote inayoonesha kuwa Yesu karibu atarudi hapa duniani?

b) Eleza kwa nini unafikiri ni ya muhimu sana.

8 B. Hebu iandike Yeremia 31:10. Ina maana gani?

*Kazi ya ziada:*
8 C. Katika Yoeli 3 tunasoma juu ya wakati ambao mataifa yote yanainuka kuipiga Israeli. Katika mistari wa 16 na 17 tunaambiwaje?